

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI



TANGAZO KWA MAAFISA UGAVI NA UNUNUZI WA UMMA

Wizara ya Fedha na Uchumi inaendesha zoezi la kuwaorodhesha Watumishi wote wanaofanya kazi za Ugavi na Ununuzi wa Umma katika Wizara na Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Wilaya, Halmashauri zote (Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya) na Wakala za Serikali. Zoezi hili pia linawahusu watumishi wanaofanya kazi hizo katika Shule za Sekondari na Vyuo mbalimbali vya Serikali, Hospitali za Mikoa na Wilaya, na vituo vyote vilivyo chini ya Maafisa Masuuli wa Makundi yaliyotajwa hapo juu. Maafisa Masuuli mnaombwa kuwajulisha watumishi wenu kujiorodhesha kulingana na utaratibu uliotumwa kwenu.

Ewe mtumishi; Ikiwa bado hujajiorodhesha, unatakiwa kuwasiliana na Muajiri wako au Mkurugenzi wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kutumia anuani inayoonekana hapo chini ili uorodheshwe katika zoezi hili muhimu. Ieleweke kwamba, katika hatua hii, zoezi haliwahusishi wajumbe wa Bodi za Zabuni, Ofisi za Mashirika ya Umma, Vyuo Vya Elimu ya Juu na Taasisi zingine zinazojitegemea. Mwisho wa kujiorodhesha ni tarehe 31 Desemba 2009.

Wizara ya Fedha na Uchumi,
S. L. P 9111,
Dar es Salaam

Simu: (22) 2129450

Fax: (22) 2129645

Barua pepe: dppu@mof.go.tz

Tangazo hili limetolewa na

Msemaji Mkuu,

Wizara ya Fedha na Uchumi